# Ugonjwa Afya na Uponyaji



MWONGOZO WA MWEZESHAJI

## Kuhudumia Afya ya Jamii yetu

Katika kukuza ufahamu wetu, kutoa huduma na msaada kwa wale wanaohitaji.

**Mpango wa muungano wa SCWA**

Toleo 2021–01b
hakimiliki © SCWA — haki zote zimehifadhiwa

info@stop–cwa.org

*translator for Kiswahili edition:*
*Marco Methuselah*

Edition 2021–01b



# Ugonjwa, Afya, na Uponyaji — Kuhudumia Afya ya Jamii yetu

Warsha ya kukuza ufahamu wetu kuhusu ugonjwa na uponyaji, ili kuweza kutoa huduma na msaada kwa wale wanaohitaji.

---

*Kama utaondoa nira ya udhalimu, na kunyoosha kidole na kuzungumza maovu! Nanyi kama mtamkunjulia mtu mwenye njaa nafsi zenu, na kuwasaidia walio katika taabu. Ndipo nuru yenu itakapong'aa gizani, nao usiku wenu utakuwa kama adhuhuri — Isaya 58:9–10.*

*Ndipo Mfalme atawaambia wale walioko upande wake wa kuume, Njooni, ninyi mliobarikiwa na baba yangu, . . . Kwa maana nilikuwa na njaa mkanipa chakula, ndipo wale wenye haki watakapomjibu, Bwana, ni lini tulikuona ukiwa na njaa tukakulisha? Nae Mfalme atawajibu, "Amina nawaambia kweli, kwa jinsi mlivyomfanyia mmoja wapo wa hawa ndugu zangu walio wadogo, mlinitendea mimi!" — Mathayo 25:34–40.*

---

## TAARIFA NA MWONGOZO KWA MWEZESHAJI

## Karibu

Lengo mahususi la mafundisho kuhusu zana za mafundisho haya na mafunzo ni kuwawezesha viongozi wa kanisa na wale walioko makanisani na katika jamii zao kuwasaidia watu, familia, na makundi ya kijamii kuendeleza ufahamu wa kibiblia kuhusu ugonjwa, afya, na uponyaji, na pia kutangaza swala la utuhumiwaji wa uchawi (dhidi ya watoto na watu wazima) unaotokana na ugonjwa na kifo. Shauku yetu ni kuona watu wakiwakinga wanajamii walioko katika mazingira magumu na kukua katika mahusiano yao na Mungu na kila mmoja kupitia Yesu Kristo.

### Makusudi

Kufikia mwisho wa mafunzo haya, inatumainiwa kuwa waliohudhuria watakuwa na ufahamu mzuri wa:

- Biblia inasema nini kuhusu ugonjwa, afya, na uponyaji;
- Biblia inasema nini kuhusu mwitikio juu ya ugonjwa na mauti;
- Njia za busara za kutafuta uponyaji;
- Njia sahihi za kuitikia endapo mmoja wao katika famia zao au jamii zao akiwa mgonjwa.

---

# Mapitio

## Muktadha

Katika jamii nyingi duniani, ugonjwa, na kifo vinaweza kunasibishwa na kazi ya nguvu za kishirikina na hasa za wachawi wanaofahamika kufanya kazi sirini, mara nyingi usiku kuwaletea wengine mabaya kupitia nguvu za asili ya ubaya. Matokeo yake, endapo mmoja wa wanajamii akiugua au kufa, swali sio "kwanini hili limetokea?" lakini swali litakuwa "nani amelifanya hili?" Wanafamilia na wanajamii – watoto kwa wakubwa - wanaweza kushutumiwa kuwa wachawi katika kibaya kilichotokea, na matokeo yake hufanyiwa vitendo vya kikatiri na kudhalilishwa, kupelekea mateso makali, majanga, hofu, wasiwasi, na kuvunjika kwa mahusiano.

Katika kesi zingine, kama mtu ataugua, msaada wa mganga wa kienyeji utatafutwa kuliko msaada wa dakitari wa hospitali na dawa zake ambazo hawaziamini. Hata kama waganga wa kienyeji wana ujuzi wa kutibu kupitia miti shamba ambayo huponyesha, lakini dawa zingine husababisha madhara kupitia ushawishi wao, njia wanazotumia, na uponyaji wanaoupendekeza. Lakini wao pia wana kikomo cha ufahamu wao wa madawa katika kusaidia. Dalili nyingi za afya huhitaji daktari na nesi mwenye ujuzi anayepatikana katika kiliniki au hospitalini ili kumpatia mgonjwa mazingira ya kupona.

Ni maombi ya SCWA kuwa mafunzo haya ya Ugonjwa, Afya, na Uponyaji yatawapatia washiriki fursa za kujadiri maswala haya muhimu na kuongozwa kuelekea katika kujifunza kupya na kupata ufahamu ambao kutapelekea kupunguza woga na kuumiza wengine, na kuongeza huduma ya upendo na msaada kwa walio wagonjwa, na hatimaye afya na ustawi katika jamii zetu kuongezeka.

## Jinsi ya Kutumia

Zana za mafunzo haya ya *Ugonjwa*, *Afya*, na *uponyaji* zinaweza kutumika kama raslimali pekee, au kama moduli ya nyongeza katika mafunzo ya Kiini cha mambo (The Heart of the Matter Hom). Mafunzo haya yako katika moduli saba za masomo zinazolenga kutoa mchango muhimu katika mabadiriko ya fikira na hatua katika makanisa na jamii katika uhusiano na matukio ya ushukiwaji wa uchawi, hasa dhidi ya watoto.

- HoM inaweza kupatikana hapa:
  — https://stop-cwa.org/resources/45

Somo hili la *Ugonjwa*, *Afya*, na *Uponnyaji* limetengenezwa ili uweze kulipanga somo katika namna unayoweza katika kundi lako na jamii yako. Kwa mfano, unaweza kuyagawa mafunzo katika sehemu mbili, nusu vipindi kwa siku au kuyafanya yote kwa siku nzima. Tunashauri kuwa jadiriana na washiriki uliowachagua ili waone mpango unaofaa zaidi kwao ikizingatia wapi na lini mafunzo yatafanyika. Hakuna haja ya kukodi ukumbi au kuwa na vifaa vya gharama. Vipindi vinaweza kufanyika katika ukumbi wowote wa jamii (chini ya mti, au katika ukumbi wa kanisa). Hauhitaji kutoa chakula, lakini utahitajika kutoa maji ya kunywa. Kila kipindi ni shirikishi hivyo ili wale washiriki wanaohudhuria waweza kushirikisha uzoefu wao na kujadiri maswala muhimu katika mafunzo haya.

## Kabla ya Warsha

Kabla ya warsha, hakikisha unaandaa yafuatayo …

- Isome notisi yote ya *Ugonjwa*, *Afya*, na *Uponyaji* ili kujizoeza na masomo yaliyomo.
- Fikiria ni nani anaweza kuwezesha warsha, na kushirikisha kitini cha *Ugonjwa*, *Afya*, na *Uponyaji* kwao ili nao wajizoeze.
- Kupitia maombi fikiria kuhusu makundi ya watu unayohitaji kuwaalika katika mkutano wako. Lengo ni kuwajenga kanisa na viongozi wa jamii ili wawagawie mafundisho haya kwa watu wengine na jamii zingine.
- Fikiria kama utatumia lugha ya wanajamii kama ndivyo, ni ipi. Hii inamaanisha utapanga mtu wa kutafsiri. Hii inategemea ni akina nani uliowachagua kuwa washiriki.
- Andaa vifaa kwa kila zoezi mapema.
  — Kwa mfano, ziandike aya na andaa karatasi ya flip chati.

## KIpindi cha Warsha

Kuna maelekezo katika somo lote ambayo yatamusaidia mwezeshaji kuwaongoza washiriki. Hakikisha kuwa unaelewa kwa ufasaha ulichoulizwa kufanya au kusema kwa kila hatua.

Fanya kila unachoweza kuhakikisha kuwa washiriki wamehusishwa na kuwa wanafursa ya kushiriki kikamilifu. Hivyo, hii itahitaji fikira makini kuhusu nini cha kuweka katika makundi madogo madogo, lugha gani ya kutumia, hakikisha kuwa na msomaji mzuri wa aya za Biblia (hasa kama kuna mchanganyiko wa elimu za watu), na fikira zingine. Ni vizuri kuzichapa rejea za aya za Biblia na maswali katika karatasi ya flip chati, kulisaidia kundi kutoandika kila kitu.

Hakikisha makundi sio makubwa sana wala madogo sana. Watie moyo waliohudhuria kuchangia mijadara, na usimruhusu mtu mmoja au wawili kutawala mjadara. Kwa kila tukio, hakikisha makundi yamechagua mtu mmoja au wawili tofauti kutoa mwitikio kwa niaba ya kundi lote.

- **Mijadara kwa wote**: Hata katika mazoezi na kila mmoja pamoja, jaribu kuhakikisha kuwa washiriki wote wamehusishwa. Ruhusu mwingiliano wa mazungumzo na chukua majibu kutoka kwa wale ambao huenda hawajioneshi. Hakikisha watu wana nafasi ya kuchangia na kuuliza maswali lakini usimruhusu mshiriki kutawala kipindi.
- **Soma kwa sauti**: Baadhi ya mazoezi (kama vile kusoma aya za Biblia) utahitaji inawahitaji kuwasomea washiriki kwa sauti. Hakikisha unaye mtu anayeweza kuongea kwa sauti inayoeleweka kwa wote kusikia.
- **Kuandika ukutani**: Baadhi ya mazoezi yanahitai kuandikwa katika ukurasa wa flip chati iliyobandikwa ukutani au katika kitu kingine. Mtafuta mmoja mwenye

mwandiko mzuri ajitolee kuandika kwa maandishi makubwa ili kila mmoja aone. (Ukimtumia mtu wa kujitolea kila wakati itakuweka wewe huru kutohusika kwenye warsha muda wote). Washiriki wasome ramani, jedwali, na kurasa zilizobakia wenyewe mwishoni mwa kipindi.

Kujizoeza na zana za warsha kutakupatia haki ya kujiamini kukifanya kila kipindi kiende bila mkwamo.

## Baada ya Warsha

Makusudi ya mafunzo haya ni kuleta mabadiriko katika fikira zetu na kuzuia matendo ya uharibifu kuendelea, kama vile ushakiwaji wa uchawi na baadhi ya matambiko ya uponyaji. Ni vyema kuhakikisha kuwa washiriki wanakiweka kile walichojifunza katika matendo. Watie moyo ili wafanye vizuri.

**Mpango Kazi Binafsi**

- Mpatie kila mshiriki mpango kazi (uliotolewa katika kiambatanisho 1) ili kuujaza. Ni vyema kuwatia moyo wajitoe kuchukua hatua kimatendo zinazolingana na mafunzo waliyoyapata kutoka katika warsha hii. Unapaswa kuwauliza kuutunza mpango kazi huu ili uwasaidie kukumbuka walichojifunza.
- Waombe washiriki ruhusa ya kuchukua picha ya kila mpango kazi ili uwe na kumbu kumbu. Unapaswa kuwaambia kuwa ungependa kujadiri pamoja nao katika miezi mitatu au miezi sita au mwaka ili kujua hatua walizopiga katika miezi ifuatayo.

**Fuatilia–Mikutano**

- Unapokutana na washiriki, unaweza kuwakumbusha jumbe muhimu kutoka katika somo. Jaribu kupima mabadiriko chanya yaliyotokea, kupitia visa kadhaa, na kuangalie matendo na fikra tofauti tofauti.

**Vyeti**

- Mwisho wa siku, watunuku waliohudhuria kila mmoja kwa cheti na wakumbushe kuhusu ushiritiki katika waarsha ya *Ugonjwa*, *Afya*, na *Uponyaji*.

## Tayari Kuendelea!

Unapoongoza warsha hii, Mungu akuwezeshe katika warsha hii na akupe baraka, hekima, na kibali!

---

# Vyanzo

Vifuatavyo ni vyanzo vilivyotumika kukamilisha andiko hili:

## Kitheolojia

- Judith Hill, "Health, Sickness, and Healing in the New Testament: a brief theology" in *Africa Journal of Evangelical Theology*, issue 26.2, pages 151–195, 2007, available online here:
  — https://biblicalstudies.org.uk/pdf/ajet/26-2_151.pdf

## Matendo

- For contextualised teaching resources on the biblical view of disability and impairments, see *Transform Disability*, published by the Bethany Children's Trust, accessible here:
  — https://bethanychildrenstrust.org.uk/resources?category=2
- SCWA's *The Heart of the Matter* (*HoM*) training resource to help change thinking and actions in relation to accusations of witchcraft, especially against children:
  - accessible here:
    — https://stop-cwa.org/resources/45
  - supplementary audio:
    — https://stop-cwa.org/resources/55
    — https://stop-cwa.org/resources/56

---

# Mawasiliano

Stop Child Witch Accusations Coalition:

« info@stop–cwa.org »